

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini

## TAARIFA KWA UMMA

### Uthibitishaji wa Madereva wa Magari ya Biashara

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, 2019, Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa magari yanayotoa huduma za usafiri kibiashara.

Katika kutekeleza jukumu hilo kisheria, Mamlaka imetengeneza mfumo wa kielektroniki utakaotumika kuwatahini madereva wa magari yanayotoa huduma za usafiri kibiashara kwa lengo la kuwathibitisha.

Mamlaka inawatangazia madereva wote wa magari yanayotoa huduma za usafiri kibiashara kuwa; kuanzia **tarehe 1 Juni, 2022** itanza rasmi kutekeleza jukumu hilo.

Ili kuweza kusajiliwa kwa ajili ya kuthibitishwa, dereva unapaswa kutuma maombi kielektroniki kupitia <https://rrims.latra.go.tz/> ili kupata nafasi ya kufanya mtihani wa kuthibitishwa.

Imetolewa na:

A blue ink signature of Gilliard W. Ngewe, consisting of several loops and a long horizontal stroke.

**Gilliard W. Ngewe**  
**Mkurugenzi Mkuu,**  
**30 Mei, 2022**